BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa, ninachukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu kwa kutujaalia uzima na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wetu. Vile vile, ninakushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuliongoza Baraza hili kwa ufanisi na nina imani kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu na kuhakikisha kuwa maendeleo makubwa yanapatikana pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** hii ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya *nane (8)*, hivyo, wananchi wana matumaini makubwa na uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Kamati yetu inawaomba wananchi waiunge mkono Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inampongeza mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa na mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Makamu wa Pili wa Rais hatua ambayo inamfanya kuwa mmoja wa wasaidizi wakuu wa mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa shughuli za Serikali yetu ya awamu ya *nane (8)*. Kamati ina imani nae katika kutekeleza majukumu yake ambayo yatailetea Zanzibar maendeleo ya haraka.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohamed pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu bila ya kuwasahau watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, ninachukuwa fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa mashirikiano makubwa wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu na kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima,naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| *9.* | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo sasa naomba nichukuwe fursa hii adhimu kutekeleza jukumu langu la msingi lililonileta mbele ya Baraza lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu wa Baraza la Wawakilishi inatekeleza Programu kuu *Saba (7)* na programu ndogo *14* ambazo zinasimamiwa na Idara *saba (7)* na Taasisi *Tatu (3).*

**FUNGU C 01: AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu na kusimamia shughuli za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kamati yetu imeridhishwa sana kwa namna Afisi hii ilivyofanikisha utaratibu

mzima wa mazishi ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki tarehe *13/02/2021* na kuzikwa kijijini kwao Mtambwe, Pemba. Vile vile, Afisi hii imeratibu vyema mipango ya shughuli za mazishi kwa mpendwa wetu aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. John Pombe Joseph Magufuli aliyezikwa kijijini kwao Chato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshauri kuwa, ni vyema ukaandaliwa utaratibu maalum wa kutekeleza ahadi zote zinazowekwa na Viongozi wetu wa Kitaifa ili ahadi hizo ziweze kutekelezwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kumekuwa na changamoto ya kujirejea kwa maafa hapa Zanzibar wakati wa mvua za masika hali inayopelekea wananchi kukosa makaazi na mripuko wa maradhi. Hivyo, Kamati yetu inashauri katika kuzuwia maafa yasitokee katika jamii, Serikali ielekeze mipango yake kwenye kuweka miundombinu itakayokinga maafa yasijirejee katika jamii yetu ambapo hatu hizo zianzie kwenye utaratibu wa ujenzi bora wa miji yetu pamoja na miundombinu ya kisasa ikiwemo barabara na mitaro ya kupitishia maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu wa Baraza la Wawakilishi kuandaa Mpango Maalum wa kukabiliana na maafa kutokana na kwamba nchi yetu kila baada ya kunyesha kwa mvua hukabiliwa na mafuriko na au maradhi ya kuambukiza ambayo hutokea katika maeneo hayo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Taasisi ya Kukabiliana na Maafa ipo zaidi kusubiri maafa yatokee ili ikabiliane nayo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuibadilisha jina Taasisi hii kuwa Taasisi ya Kuzuia Maafa badala yake ili iwe na jukumu la msingi la kuzuia maafa yasitokee nchini kinyume na ilivyo sasa kwa Taasisi hiyo kusubiri maafa yatokee ndiyo ifanye kazi.

**FUNGU C02: BARAZA LA WAWAKILISHI**

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni moja ya Muhimili Mkuu wa nchi ambao una jukumu kubwa la kutunga Sheria, kufuatilia utendaji wa Serikali na kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali ili kuhakikisha kuwa mahitaji na maendeleo ya wananchi yanapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaipongeza sana Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza vyema taratibu za uzinduzi wa Baraza jipya la Kumi pia kufanya uteuzi wa viongozi wa Baraza pamoja na wa Kamati kwa mujibu wa taratibu na sheria za Kibunge.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati inashauri Baraza liingiziwe fedha katika kila robo mwaka ili liweze kutekeleza vyema majukumu yake iliyojipangia.

**FUNGU C03: TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Tume hii kutokana na kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia vyema Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliofanyika

*Oktoba, 2020* kwa kuhakikisha unakuwa wa Haki na Amani licha ya kuwepo changamoto yao ya uhaba wa vyombo vya usafiri.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati yetu inashauri ndani ya bajeti hii zitengwe fedha zitakazowawezesha kununua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu hayo ya Tume hadi katika wilaya zetu za Unguja na Pemba.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie Bajeti hii na hatimae waidhinishie Wizara ya Katiba na Sheria makadirio na makisio ya fedha zote zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2021/2022* kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** *kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………………………….

***(Hassan Khamis Hafidh)***

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**